

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA UKEREWE**  
**MKOA WA MWANZA**

Simu:+255 282 515056 /+255 685 304646

Barua pepe:[ps@ukerewedc.go.tz](mailto:ps@ukerewedc.go.tz)  
Tovuti: [www.ukerewedc.go.tz](http://www.ukerewedc.go.tz)  
Unapo jibu tafadhali taja



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaj(W)  
S.L.P. 41,  
NANSIO/UKEREWE.

Kumb Na:EA141/272/

22 / 07/2021

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MUDA YA  
KUKUSANYA MAPATO YA HALMASHAURI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Ukerewe anakaribisha maombi kutoka kwa wananchi waishio wilayani Ukerewe wenyе sifa na uwezo wa kujaza nafasi za kazi 70 kwa ajili ya kufanya kazi ya kukusanya mapato katika vituo mbalimbali vya kukusanya mapato.

**MAJUKUMU YA KAZI YATAKUWA:**

- 1.Kukusanya ushuru katika Magilio,Mialo Masoko na maeneo mengine
- 2.Kuwasilisha fedha zilizokusanya benki mara tu baada ya kuzikusanya.
- 3.Kuandaa taarifa za makusanyo pamoja na kutuma taarifa katika mfumo wa mapato

**MASHARTI YA JUMLA**

1. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania wenyе umri kati ya miaka 18 hadi 45
2. Muombaji ajue kusoma, kuandika na kuhesabu.
3. Muombaji awe mkazi wa Ukerewe.
4. Muombaji aambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.
5. Maombi yote yapitie kwa **Mwenyekiti wa Kijiji na Mtendaji wa kijiji wa eneo analotoka.**

6. Muombaji aambatanishe majina ya wadhamini (Referees) wawili ambapo sharti mmojawapo awe mtumishi wa umma, kutoka katika eneo lake la makazi, yakiwa na anuani na namba za simu za kudumu.

### **MASHARTI MENGINEYO**


1. Awe na uelewa wa kutumia komputa au simu aina ya “smart phone”
2. Awe mkazi wa wilaya ya Ukerewe na awe tayari kufanya kazi kwenye visiwa/vijiji vya Ukerewe kwa gharama zake.
3. Kazi hii ni ya muda ,hivyo itakuwa ya mkataba kwa muda wa miezi mitatu (3)

**MALIPO:**Watakaopata kazi hii watalipwa kamisheni ya 10% ya fedha watakazo zikusanya na kuwasilisha benki.

Wananchi watakaopendelea kuomba nafasi hii ya kazi wanaweza kuandika kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza na maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:

Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe,  
S.L.P 41,  
**NANSIO/UKEREWE**

**Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 30 Julai, 2021 saa 9:00 Alasiri**

  
Ester A. Chaula  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**UKEREWE**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**UKEREWE**